


# SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



EU UNIVERSE  
AWARENESS

## Ulimwengu Usioonekana Wafunuliwa



Picha za angani mara nyindi huwa za kupendeza. Kitu kimoja kizuri kuhusiana nazo ni kwamba huonyesha vitu visivyoonekana kwa macho ya binadamu. Picha hii pia ipo hivyo. Kati kati kabisa ya picha linaonekana shimo jeusi, liitwalo super-massive black hole. Kulifanya shimo hili liliilo na uzoefu mkubwa wa kuficha vitu kuwa gumu zaidi kulisoma, limejificha chini ya wingu zito la vumbi na gesi katika kiini cha galaksi liliromo! Hata madoa ya rangi rangi unayoyaona yanatoa miale ya mwanga ambayo macho yetu hayawezi kuiona. Rangi ya pinki inaonyesha rangi ya radio, na ile ya X-ray inaonekana kwa rangi ya blu.

Shimo jeusi si chochote zaidi ya sehemu iliyo wazi, usifanye jina likupumbaze. Ni sehemu ndogo iliojaa maada nyindi sana – hili hapa lina uzito zaidi ya mara milioni 100 ukilinganisha na ule wa Jua letu! Kitu chochote kinachozunguka karibu na shimo jeusi hufyonzwa ndani yake na hakiwezi kutoroka na mwanga ukiwemo. Na hii ndio sababu inayotufanya fusiweze kuyaona mashimo meusi, hayaonekani hata kwa telescopes zinazoweza kufambua miale ya X-ray, mawimbi ya radio na aina nyindigine za mwanga.

Njia pekee ya sisi kuliona shimo jeusi ni kwa kugundua athari yake kwa vitu vingine. Kwa mfano, katika picha hii, mabaka ya rangi ya blu, katika kingo za galaksi yanaonyesha sehemu zenye mikondo yenye nishati nyindi inayovutwa kuelekea kati gimba la vumbi. Mikondo hiyo imetengenezwa na chembe chembe za maada ambazo zilipashwa joto zilipokuwa zinavutwa katika shimo jeusi. Tendo hili lilizipatia n̄guvu maada na kuzifanya zikimbie kutoka kwene shimo katika mwendo kasi wa maili milioni moja kwa saal. Aina mbili za mikondo inayofanana na hiyo inaweza kuonekana, inarukia upande wa Kaskazini na Kusini wa galaksi.

### COOL FACT

Mashimo meusi sio vitu pekee ambavyo havioneekani kwa macho yetu. Wanaastronomia bado hawajafumbua fumbo la vitu visivyoonekana "nishati nyeusi" dark energy na "maada nyeusi" dark matter ambavyo vyote vikiunganishwa hutengeneza asilimia 95% ya Ulimwengu! Ni karibu chini ya 5% ya Ulimwengu ndio imetengenezwa na vitu vya kawaida!



More information about EU-UNAWE  
Space Scoop: [www.eu-unawe.org/kids/](http://www.eu-unawe.org/kids/)